JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA
Tovuti: www.hlpc.go.tz
Barua pepe: hlpc@afya.go.tz

# TANGAZO

## MAOMBI YA USAJILI WA AWALI NA KUCHAGUA KITUO CHA UTARAJALI KWA WAHITIMU WA NGAZI YA SHAHADA YA SAYANSI YA MAABARA YA AFYA

Ofisi ya Msajili, Baraza la Wataalam wa Maabara inapenda kuwataarifu wahitimu wa Shahada ya Maabara za Afya kufanya maombi ya usajili wa awali (Provision Registration) ili kuwawezesha kuchagua kituo cha utarajali. Wahitimu wote wanaohitaji usajili wa awali wanahimizwa kufanya maombi mapema kabla ya dirisha kufungwa. Waombaji wa usajili wa awali wanatakiwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo kwenye mfumo ***hprs.moh.go.tz***;

- Cheti cha kuzaliwa
- Cheti cha elimu ya sekondari
- Cheti cha matokeo ya chuo (transcript) au cheti cha taaluma cha chuo
- Cheti cha uthibitisho kutoka TCU (kwa waliosoma vyuo vya nje ya nchi)
- Barua ya uthibitisho kutoka chuoni (Waliosoma nchini)

Aidha, Dirisha la kuchangua vituo cha utarajali litafunguliwa tarehe 20.03.2025 saa 03:00 asubuhi na kufungwa tarehe 21.03.2025 saa 03:00 asubuhi. Mambo muhimu ya kuzigatia kwa waombaji wa kituo cha utarajali;

- Mhitimu awe amefanya maombi ya usajili wa awali kabla kwa kutumia akaunti ya ngazi ya shahada.
- Chaguo la kituo au kubadilisha kituo cha utarajali inafanywa na mwombaji kabla ya dirisha kufungwa.
- Watakaochagua vituo wafike ofisi ya Msajili, Baraza la Wataalam wa Maabara tarehe 27.03.2025 saa 2:00 asubuhi kwa ajili ya kuchukua barua na nyaraka nyingine muhimu za kuanza utarajali.

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara linawatakia utekelezaji mwema.

Kwa msaada zaidi piga simu 0734005777

Imetolewa na:

Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
04.03.2025

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
04 MAR 2025
P.O.Box 743
DODOMA